
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO
SHULE YA SEKONDARI KIMOKOUWA,
S. L. P 8523,
NAMANGA-ARUSHA.
E-Mail: kimokouwasec@gmail.com
**Simu Na: 0753198562**

*Kwa MAWASILIANO ZAIDI:*
*MKUU WA SHULE: 0753198562*
*MAKAMU MKUU WA SHULE: 0760475053*
*MWALIMU WA MALEZI(MATRON):0699252075/0754299068*
*MZAZI/MLEZI WA:………………………………………………………………..*

**YAH: - MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI KIMOKOUWA MWAKA 2026**

***1. Karibu Shuleni Kimokouwa.***

Uongozi wa shule ya sekondari Kimokouwa unapenda kukupongeza kwa kufanya vizuri na kuchaguliwa kijiunga na KIDATOCHA KWANZA mwaka 2026.
**"*STRIVE FOR THE BEST* (*PAMBANIA KILICHO BORA ZAIDI*)"** Maneno haya ndiyo **KAULI (MOTO)** au mwongozo wa shule yetu. Kama umeridhia kujiunga na shule hii, huna budi kuitafakari kauli hiyo na kuichukulia kwa uzito unaostahili.
Shule ya Sekondari Kimokouwa ipo umbali wa kilometa Tisini na mbili (92) tu kutoka kituo kikuu cha mabasi ya Arusha mjini. Usafiri kutoka mjini Arusha unapanda Noah za kwenda na kumwomba Dereva akushushie Kimokouwa kituo cha Ngulupa utaona kibao cha shule kilichopo mbele kidogo tu ya Kizuizi cha Askari ukitokea Arusha.
Nauli ni shilingi 7**,000/= toka stendi kuu ya Arusha .** Kwa wanaotokea Namanga na Longido Usafiri wa daladala pia unapatikana kwa shilingi 1500/= **Unatakiwa** kuripoti shuleni **tarehe** 10/01/2026
Tafadhali nakuomba wewe na mwanao msome maelekezo haya kwa kina na kisha mkamilishe yale yote yanayotakiwa. Pia endelea kumshauri mwanao juu ya kutumia nafasi hii aliyoipata vema ili lengo na azma yake itimie.pia ukikutana na changamoto yoyote ile waweza kupiga kwa mkuu wa shule au namba yoyote ile iliyoonyeshwa hapo juu kwa msaada. Nakutakia maandalizi mema na karibu Kimokouwa Sekondari.




JOSEPH J. AYO
MKUU WA SHULE (0753198562)

***2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-***

**A. Sare ya shule:- wasichana**

I. **Sare ya darasani:-**

❖ Sketi mbili rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) mshono wa rinda box urefu wa sketi ifunike vifundo vya miguu (aje nazo)

❖ Mashati mawili meupe aina ya tomato, mikono mifupi, yenye "collar" na mfuko kwa kila shati **(Aje nayo** ). Tai ndefu ya rangi ya dark blue yenye miraba meupe (aje nayo pia zinapatikana duka la karibu na shuleni kwa sh. 3000)

❖ Viatu vyeusi vya kufungwa kwa kamba, vyenye visigino vifupi (muundo kama viatu vya kiume). ( **Aje navyo** ).

❖ Soksi nyeupe jozi mbili (02) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi ( **Aje nazo** ).

❖ Sweta moja rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) aje nayo au **yenye nembo ya shule inapatikana duka lilolopo karibu na shuleni** - kwa malipo. (20,000 Tsh).

II. ) **Sare ya kazi za nje:-** Gauni rangi ya bluu iliyokolea ( **aje nayo** ) na

III. T - shirt 2 rangi bluu iliyokolea, moja yenye collor na isiyo na collor. Aje nazo au **yenye nembo ya shule** zinapatikana katika duka lililopo karibu na shule kwa gharama ya sh. 15000.

IV) **Sare za michezo:-** Raba nyeusi, Track suit rangi bluu bahari (light blue). Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo hivyo aje nazo

d) Kwa watakaovaa **hijab** , waje na mashati mawili meupe ya **mikono mirefu** (aina Tomato) na **juba** rangi nyeupe **linalofunika mikono**.

Kwa upande wa **sare za kazi za nje** aje na juba la **rangi ya njano** linalofunika mikono.

a) Wanafunzi watavaa sare ya darasani **wakati wa vipindi** na sare ya kazi za nje **baada ya muda wa vipindi**. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA** , hivyo **asije nazo**.

***weka alama kwenye kila nguo au kifaa chako sehemu rahisi kuonekana ili kutambua ichukuliwapo na asiye mmiliki.***

Iv) **vifaa na mahitaji ya bwenini**

(i) Ndoo mbili (02), moja (01) ya kuogea/kufulia na moja (01) ya kuhifadhia maji.
(ii) Kanga au kitenge (jozi moja tu)
(iii) Taulo, mswaki na dawa ya meno, sabuni na mafuta ya kupata.
(iv) Godoro futi 2 1/5 x 6
(v) Tochi ya kumsaidia wakati umeme ukikatika.

V) ***Vifaa vya usafi: -***

(i) Toilet/scrubing brush (01), Softbroom (fagio laini) (01), hard broom (fagio la brashi ngumu 01),
(ii) Rubber squeezer (fagio la kusukumia maji 01), jembe jipya na mpini wake (01),
(iii) Dawa ya kusafishia vyoo lita moja.

## B. Sare ya shule:- wavulana

IV. **Sare ya darasani:-**

❖ Suruali mbili rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) ndefu na zisizobana.

❖ Mashati mawili meupe aina ya tomato, mikono mifupi, yenye "collar" na mfuko kwa kila shati **(Aje nayo** ). na,

Tai ndefu ya rangi ya dark blue yenye miraba meupe (aje nayo na pi zinapatikana duka la karibu na shuleni kwa sh. 3000).

- ❖ Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba, vyenye visigino vifupi . ( **Aje navyo** ).
- ❖ Soksi nyeusi jozi mbili (02) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi ( **Aje nazo** ).
- ❖ Sweta moja rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) isiyo na mistari. aje nayo au **yenye nembo ya shule inapatikana duka lilolopo karibu na shuleni** - kwa malipo. (20,000 Tsh).

II.) **Sare ya kazi:-** Suruali ya blue bahari ndefu isiyobana (aje nayo) na T - shirt 2 rangi ya bluu iliyokolea.Moja iwe na collor na isiyo na collor.Aje nazo au **yenye nembo ya shule** zinapatikana **duka lililopo karibu na shule** kwa malipo ya shilingi 15000/= kwa tisheti moja.

III) **Sare za michezo:-**

- ➢ Raba nyeusi, Track suit rangi bluu bahari (light blue). Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo hivyo aje nazo.
- ➢ Bukta mbili za rangi ya (blue iliyokolea) dark blue.

N:B; Wanafunzi watavaa sare ya darasani **wakati wa vipindi** na sare ya kazi **baada ya muda wa vipindi**. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA** , hivyo **asije nazo**.
***weka alama kwenye kila nguo au kifaa chako sehemu rahisi kuonekana ili kutambua ichukuliwapo na asiye mmiliki.***

Iv) V**ifaa na mahitaji ya bwenini wavulana**

- ◆ Ndoo mbili (02), moja (01) ya kuogea/kufulia na moja (01) ya kuhifadhia maji.
- ◆ Taulo, mswaki na dawa ya meno, sabuni na mafuta ya kupata.
- ◆ Mashuka mawili ya blue iliyokolea (dark blue).(weka alama ili kutambua ichukuliwapo na asiye mmiliki)
- ◆ Godoro futi 2 1/5 x 6
- ◆ Tochi ya kumsaidia wakati umeme ukikatika.

V) ***Vifaa vya usafi: -***

(i) Toilet/scrubing brush (01), Softbroom (fagio laini) (01), hard broom (fagio la brashi ngumu 01),
(ii) Rubber squeezer (fagio la kusukumia maji 01), jembe jipya na mpini wake (01),
(iii) Dawa ya kusafishia vyoo lita moja.

**MAHITAJI MUHIMU MENGINEYO KWA WANAFUNZI WOTE:**

(i) Aje na ream bunda **mbili(2) za karatasi nyeupe (A4 Mond**i). Kwa ajili ya mazoezi toshelevu ya mwaka. ***Mwanao hatapokelewa asipoleta rimu mbili A4 mondi kwa ajili ya uchapaji wa mitihani.***
(ii) Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yako.
(iii) Mzazi wasiliana na duka la vitabu lililokaribu yako ili kupata vitabu rejea vinavyoendana na mtaala mpya wa 2023.
(iv) FILE (faili la kaki moja) kwa ajili ya kutunzia mitihani ya majaribio ya ndani na nje.

(v) Sanduku kwa usalama safarini na shuleni. Inashauriwa ununue sanduku kubwa la **BATI** la kutosha vifaa vyako vyote. (tunapokea sanduku moja tu).
(vi) Kama una **Bima ya afya** njoo nayo, kama huna mzazi au mlezi **mkatie mwanao Bima ya Afya.**
(vii) Vyombo vya kulia chakula ni Sahani, container dogo la chakula, kikombe cha nusu lita ( vyote vya rangi ya blue iliyokolea) na kijiko.

**Ili kuleta ulinganifu sare zifuatazo zinapatikana katika duka lililopo karibu na shuleni kwa gharama zifuatazo:**-
i. T - shirt mbili zenye nembo @ shilingi 15,000/= jumla kwa zote mbili ni shilingi 30,000/=
ii. Sweta moja (01) rangi ya dark bluu lenye Nembo - shilingi 20,000/=
Iii. Nembo mbili kwa ajili ya mashati mawili (02) na track suit - shilingi 5,000/=
Iv. Kitambulisho cha mwanafunzi - shilingi 5,000/=

***4 .AFYA YA MWANAFUNZI:-***
Mara upatapo barua hii mwone **Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali** iliyo karibu nawe, ili upimwe kuthibitisha kuwa una afya ya kutosha kusoma masomo ya sekondari. Fomu maalum imeambatanishwa na barua hii. Mara utakapofika shuleni ioneshe ikiwa imejazwa. Shule haitoi chakula maalumu (special diet) kwa wagonjwa. Hata hivyo ni:- **Ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni.**

**5. SHERIA ZA SHULE:**
Zifuatazo ni sheria za shule kinyume nazo kutasababisha Mwanafunzi kuadhibiwa, kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule kabisa.
***A) MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUADHIBIWA***
1.) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote.
2.) Marufuku kuingia kuingia sehemu zifuatzao bila ruhusa
   a. Ofisi ya walimu
   B. Ofisi za shule
   C. Maabara
   D. Jikoni
   E. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

3.) Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote.
4.) Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.
5.) Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani na wakati wa kujisomea.
6.) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua, ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na **Mkuu wa Shule.**
7.) **Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, "earphones" pamoja na redio**.
8.) Mwanafunzi haruhusiwi **kupiga simu popote** bila kibali cha uongozi wa shule , ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia **ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule** na **Ofisi ya Malezi** au mwalimu aliyepewa jukumu hilo na mkuu wa shule.

9.) Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani.

10.) Mwanafunzi haruhusiwi **kufanya mazungumzo** na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani, au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na **uongozi wa shule**.

11) Kutoheshimu au kutothamini kazi za aina zote zinazotolewa na uongozi wa shule.

12.) Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl, nywele za bandia, mapambo kama bangili hereni, mikufu n.k. havitakiwi kabisa shuleni.** Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na **kucha ndefu wala kujipamba**.

13.) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani, (Kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi)

14.) Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika kwa kupewa kibali toka kwa mwalimu wa afya)

15.) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi wakati wote** wawapo shuleni, urefu **unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana**. Hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven. Mwanafunzi aje na fedha ya kunyoa muhula mzima shilingi 5000/= ili kuepusha ufugaji wa nywele maana atanyolewa pindi tu nywele zitakaporefuka kwa mtindo unaokubalika.

16.) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

17.) Ni marufuku **kumruhusu mgeni** kufika katika **eneo la mabwenini**.

18.) Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa **kwa kumsalimia**.

19.) Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa **kumwombea ruhusa mwanafunzi** kama kuna tatizo. Pia ndiye **atakayekuja shuleni** pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

20.) Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka **kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule**. Hakuna **ruhusa yoyote itakayotolewa mapema** kabla ya **siku rasmi ya kufunga shule**.

21.) Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la nidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba,shangazi, kaka.

22.) LUGHA YA MAWASILIANO SHULENI NI KIINGEREZA. Ni marufuku kutumia Kiswahili kuwasiliana isipokuwa wakati wa somo la Kiswahili na somo La Historia na maadili tu. Practice make it perfect. Hii itasaidia ujifunzaji na uelewa kwa kuwa masomo mengi hufundishwa kwa lugha ya kiingereza.

***B) MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE:***

***M****akosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja:*

a. Kutukana/kutumia lugha chafu, kumpiga mwalimu au mwanafunzi mwenzake

b. Kupigana na mwanafunzi mwenzake.

c. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.

d. Kuoa au Kuolewa.

e. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, na mwanafunzi na mwalimu au mtumishi yeyote.

f. Ulevi wa aina yoyote ikiwemo, pombe, sigara, madawa ya kulevya na Bangi
g. Kujihusisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja, yaani ushoga na usagaji.
h. Kutoka nje ya eneo la shule bila kibali au ruhusa kutoka kwa mkuu wa shule, makamu, mwalimu wa nidhamu na mwalimu wa zamu.
i. Kutoa taarifa zisizo sahihi au chonganishi kwa wanafunzi wenzake, walimu au wazazi au mtu yoyote.
j. Kugoma,Kuchochea au kusababisha mgomo au maandamano shuleni.
k. Kumiliki simu au vifaa vyenye kutumia umeme.
l. Kumiliki vifaa vyenye ncha kali bwenini mfano panga, kisu na sime.
m. Kukataa adhabu makusudi.
n. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUPITIA SHERIA ZA SHULE;

Mimi...................................................................................................nakiri

Nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa hivyo basi ninaahidi “nitazifuata sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoelekezwa. Aidha ninaamini kuwa sheria na taratibu zote zipo kwa nia ya kunisaidia katika nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu na taaluma” kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe zidi yangu.

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa,
nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya taifa kwa jumla.

Jina la mwanafunzi:………………………………………………………………. sahihi…………………….
Jina la mzazi/mlezi: ………………………………………………………………. sahihi…………………..
Tarehe :……………………………….

KIMOKOUWA SECONDARY SCHOOL, P.O BOX 8523, NAMANGA-ARUSHA**.**
DATE ........................... Ref. No............................................…

TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI MPYA

SEHEMU A:

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………….. (picha 1 passpot size)
Dini…………………………………..

SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/ WALEZI NA JAMAA:

(i) Jina la Baba………………………………………………. (picha 1 passpot size)
Anaishi Kijiji/mtaa…………………………………………………. kata ………………………
Kazi yake ni ………………………………………………………. anwani yake ni………………..
Namba yake ya simu ni……………………………….

(ii) Mama yangu anaitwa………………….. (picha 1 passpot size)
Anaishi Kijiji/mtaa…………………………………………………. kata ………………………
Kazi yake ni ………………………………………………………. anwani yake ni………………..
Namba yake ya simu ni……………………………….

(iii) Jina kamili la mzazi/mlezi anayemuhudumia mwanafunzi ikiwemo

(picha 1 passpot size kwa kila mlengwa)

**PART A:-** To the Medical
Officer, ...................................................... .....................................................
...
**REF: .......................................................................................................................**
. Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a boy/girl for Secondary Schools' education.

a). Eye sight b). Hearing c). Limbs d). Speech e). Venereal disease f). Leprosy g). Epilepsy
Neurosis
Other serious diseases
Pregnancy
.

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER** )
I have examined the above named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

a). Eye sight .........................
(b). Leprosy............................................ c). Hearing ...................................
d. Epilepsy........................................... e). Limbs .........................................
f). Neurosis........................................... g). Speech ......................................
h). Other serious diseases...................... i). Venereal diseases ......
j). Pregnancy.........................................
Name............................................................ Signature............................
Date............................
**STATION** ...........................................................
**DESINATION** ..................................................
**N.** I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.
KIMOKOUWA SECONDARY SCHOOL